**HOTUBA YA MHE. ENG. MTEMI MSAFIRI SIMEON, MKUU WA WILAYA YA KWIMBA WAKATI WA SHEREHE YA KILELE CHA MAADHIMISHO YA WIKI YA MAZIWA KIWILAYA KATIKA KIWANJA CHA KWIDECO NGUDU TAREHE 01 JUNI, 2017**

- Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya,
- Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya,
- Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya,
- Viongozi wa dini na vyama vya siasa,
- Watendaji wote wa Serikali mliopo hapa,
- Wananchi wote mliohudhuria maadhimisho haya,
- Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuwashukuru waandaaji wa maadhimisho haya ndani ya Wilaya kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu. Aidha , niwapongeze kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho licha ya changamoto kadhaa mlizokumbana nazo. Niwashukuru pia wananchi na wote ambao mmeona umuhimu wa siku ya leo mkaamua kuacha shughuli zenu na kuhudhuria maadhimisho haya.

Ndugu wananchi, kama tulivyofahamishwa, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa Tanzania, kila mwaka huandaa maadhimisho ya Wiki ya Maziwa. Maadhimisho haya hufanyika kati ya wiki ya mwisho ya mwezi Mei na wiki ya kwanza ya mwezi Juni. Kwa mwaka huu maadhimisho haya yanafanyika kitaifa Mkoani Kagera na kilele chake ni leo tarehe 01/06/2017. Ikumbukwe kuwa siku hii ndiyo pia Siku ya Maziwa Duniani. Kauli mbiu ya Siku ya Maziwa mwaka huu inasema***: "Kunywa Maziwa, Jenga afya, furahia maisha"***

Ndugu wananchi, madhumuni ya Siku ya Maziwa ni:

- Kuelimisha umma juu ya matumizi ya maziwa kama chakula bora katika kujenga afya ya binadamu kwa watu wa rika zote na juu ya faida za maziwa.
- Kuelezea juu ya faida za maziwa katika mwili wa binadamu.
- Kushawishi watunga Sera kuona umuhimu wa kuinua tasnia ya Maziwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuondoa umaskini kwa wananchi wetu.

- Kuwaelimisha wadau wa tasnia ya maziwa na hasa wafugaji kuongeza uzalishaji na ubora wa maziwa na bidhaa zake zinazotengenezwa nchini.
- Kuwaelimisha wadau umuhimu wa kujiunga na vyama vya ushirika vya kuzalisha maziwa na bidhaa zake kwa wingi na ubora unaokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.
- Kutoa fursa ya wadau kukutana na kubadilishana uzoefu wa uzalishaji wa maziwa katika kuendeleza tasnia ya maziwa Tanzania.

MAADHIMISHO KIWILAYA:

Madhumuni yetu kiwilaya ni kutumia maadhimisho haya kuwa chachu kwa wafugaji wetu kuhamasika kutumia fursa walizonazo kuifikisha Kwimba kwenye hatua ya juu kabisa katika kuzalisha maziwa mengi na bora. Hii itajumisha suala la kuwa na viwanda vidogo vya usindikaji wa maziwa na mazao yake, na kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wakubwa pia ili kutengeneza soko la ndani la maziwa yetu.

Fursa tulizo nazo kwenye Wilaya yetu ya Kwimba ni pamoja na:

- MIFUGO: Tunao ng’ombe wa asili wapatao 390,991, ng’ombe wa maziwa wapatao 122. Ng’ombe hawa wakitunzwa kwa kanuni za ufugaji bora wenye tija ikiwa ni pamoja na kutumia ubadilishaji wa ng’ombe wa asili ili kupata ng’ombe walio bora kwa kutumia madume bora na uzalishaji kwa chupa(uhamilishaji), tutakuwa na uzalishaji mkubwa na wa kutosheleza soko la ndani na hata kuuza nje ya Wilaya.
- WATAALAM: Wafugaji wetu wana fursa kubwa ya kupata elimu juu ya ufugaji bora wenye tija kwa wataalam wetu wa mifugo ambao pamoja na uchache wao bado wanaweza kufikisha elimu hiyo kwa wafugaji japo kwa kuhudumia maeneo makubwa kunakofanya wafugaji wengi kutofikiwa kwa wakati. Kati mahitaji ya wataalamu wa mifugo 139 wanaohitajika, waliopo ni 34 tu na hivyo kuwa na upungufu wa wataalamu 105. Hata hivyo Serikali itaendelea kuajiri wataalam lengo likiwa angalau kila kijiji kiwe na mtaalam wa mifugo. Pamoja na kutoa elimu ya ugani kwa wafugaji wataalam hawa pia hutoa huduma za afya ya mifugo.

- ARDHI: Ardhi yetu ni kubwa inayoweza kutumika kuzalisha malisho ya mifugo nafaka inayoweza kutumika kutengeneza vyakula vya nyogeza (Suppliments). Hata hivyo hatuna budi kuitunza ardhi hii. Hii ni pamoja na kutoharibu mazingira kwa kukata miti ovyo na bila kupanda miti mingine na kuitunza. Tukifanya hivyo tutasababisha ardhi ya wilaya yetu kugeuka jangwa na hivyo kutokufaa kwa shughuli za ufugaji kwakuwa kutakuwa na upungufu wa malisho na maji.
- MIPANGO MIZURI YA MAENDELEO: Serikali na Halmashauri yetu kwa ujumla kupitia Mipango na Bajeti ya kila mwaka hutekeleza miradi mbalimbali kuendeza sekta ya mifugo ikiwemo miundombinu mbalimbali ya mifugo kama ujenzi na ukarabati wa majosho, malambo, mabirika ya kunyweshea maji, visima vya maji, minada n.k. Hata hivyo hapa kuna changamoto kidogo ya miundombinu. Kwa mfano kati ya majosho 119 yanayohitajika, tuna majosho 32 na kati ya hayo ni majosho 12 pekee yanayofanya kazi.

Hizi ni baadhi tu ya fursa nyingi tulizo nazo za kuendeleza tasnia ya maziwa kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi  na kuondoa umaskini.

Ndugu wananchi, nimalizie hotuba yangu kwa kufupisha yale niliyoyasema. Wilaya yetu inao ng’ombe wengi kwa idadi niliyoitaja hapo awali. Ng’ombe hao wakifugwa kitaalamu, nina uhakika kuwa watakuwa na uwezo wa kutoa maziwa yatakayotosheleza mahitaji yetu ya ndani na hata ziada kuuza nje ya wilaya. Kwa kufanya hivyo tutasaidia pia uwepo wa viwanda vidogo vodogo kwani maziwa haya yanahitajika kuwekwa katika ubora wa kuvutia watumiaji. Niwaase wananchi wote wa Wilaya ya Kwimba, tuwe na mazoea kunywa maziwa kwa afya yetu badala ya kunywa vinywaji vingine ambavyo ni hatari kwa afya yetu.

Baada ya kusema ya kesma hayo niwashukuru kwa maandalizi na mahudhurio yenu.

***“KUNYWA MAZIWA, JENGA AFYA, FURAHIA MAISHA.”***

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**